# BRELA

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

ISSN: 000401 | Toleo Na. 09 | Machi - julai, 2024

# BRELA YATOA GAWIO KWA SERIKALI KWA TAASISI ZA UMMA



# MSAMAHA WA ADA YA UWASILISHAJI WA NYARAKA ZA KAMPUNI ZILIZOSAJILIWA KABLA YA MWAKA 2018



Msajili wa kampuni anapenda kuwataarifu Wamiliki, Wakurugenzi na Makatibu wa kampuni kwamba baadhi ya kampuni zimekuwa hazitekelezi wajibu wao wa kisheria wa kuwasilisha kwa Msajili wa kampuni Taarifa za Mwaka na Mizania (Annual Returns and Audited Accounts) za Kampuni kama Sheria ilivyoelekeza.

Sheria pia, inazitaka kampuni za Kigeni (Foreign Companies) kuwasilisha Mahesabu yake ya Mwaka kila mwisho wa mwaka (Calendar Year).

Taarifa hizi zinatakiwa kuwasilishwa kwa Msajili wa kampuni kila ifikapo tarehe na mwezi ambao kampuni ilisajiliwa (anniversary of incorporation) au tarehe nyingine yoyote ambayo Kampuni itakuwa imeichagua na kumtaarifu Msajili wa kampuni nae akaridhia. Sharti hili ni kwa mujibu wa Kifungu cha 128 cha Sheria ya kampuni, Sura 212.

Msajili wa kampuni anapenda kuwafahamisha na kuwakumbusha kwamba, kuanzia sasa, Taarifa za Mabadiliko yoyote yanayoletwa na kampuni hayatafanyiwa kazi mpaka Kampuni husika itakapokuwa imewasilisha Taarifa zake za Mwaka.

Taarifa za Mwaka na Mahesabu ya Mwaka kwa kampuni za kigeni (Foreign Companies) husaidia kutoa taswira halisi ya Kampuni, hivyo humuwezesha Msajili wa kampuni kuwa na taarifa sahihi za Kampuni husika.

Kampuni zinahimizwa kuwasilisha Taarifa za Mwaka ili kuepuka usumbufu unaoweza kutokea wakati kampuni inawasilisha taarifa za mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika kampuni.

# YALIYOMO


05




BRELA yatoa gawio

06



BRELA yasaini makubaliano na taasisi nne za Serikali

08



BRELA watakiwa kufungua mlango wa kuelimisha umma

09




Tanzania yasaini mkataba wa kihistoria

13




Brela yatoa elimu maonesho ya miaka 60 Ya muungano

# TAHARIRI



Ninayo furaha kubwa kukukaribisha kwa mara nyingine tena katika Toleo la Tisa la Jarida letu la BRELA. Katika kipindi hiki cha robo ya nne na ya mwisho ya Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Taasisi imepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau wake wakiwemo viongozi wa juu wa kidini, wasanii na watu mbalimbali maarufu nchini. Hii kwetu ni faraja kubwa katika jitihada za kuimarisha ushirikiano na wadau wetu na kuongeza nguvu za kuitangaza BRELA na huduma zake ndani na nje ya Tanzania ikiwa ni lango la kibiashara. Hivyo, Toleo hili limebeba habari mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za urasimishaji biashara nchini.

Aidha, azma yetu ni kusimamia maadili yetu ya msingi na nguzo kuu ikiwa ni uadilifu wa hali ya juu na kujali wateja kwa kuhakikisha wateja na wadau wetu wote wanafikiwa na huduma zetu bora zinazozingatia weledi na viwango vya hali ya juu. Juhudi za makusudi zinafanywa na Wakala kuhakikisha huduma zetu zinakuwa za kisasa zaidi na zinapatikana kwa urahisi kwa kuzingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia. Ni dhahiri shahiri kuwa, BRELA inaendelea kuboresha mifumo yake ya kiutendaji. Hivi karibuni BRELA imepata tuzo katika kipengele cha taasisi bora ya Serikali kidigiti kutambua mchango bora katika mageuzi ya kidigiti nchini Tanzania. Na hii ni fahari kubwa kwa Wakala katika kuongeza ari ya8 kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa ili kujenga mazingira bora zaidi na wezeshi ya biashara hapa nchini.

Katika anga za kimataifa, Tanzania kupitia BRELA ilishiriki mkutano wa kidiplomasia wa ukamilishwaji wa Sheria ya Kimataifa ya Miliki Ubunifu katika Rasilimali za Kijenetiki na Maarifa ya Jadi yanayohusiana na Rasilimali za Kijenekiti uliofanyika katika Ofisi za Makao Makuu ya Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO) jijini Geneva, Uswisi. Sheria hii inalenga kuhakikisha mfumo wa ulinzi wa Miliki Ubunifu unatambua matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki na Maarifa ya Jadi ili kuwanufaisha wamiliki wa rasilimali hizo.

BRELA inatambua na kuthamini nafasi ya viongozi wa dini katika kusimamia suala zima la maadili na uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika kuliishi hili, Taasisi iliandaa Iftar. Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania Dkt. Sheikh Abubakar Zubeir Bin Ali Mbwana alishiriki akiwa mgeni rasmi katika tukio hilo na kuhimiza juu ya uadilifu na kuzingatia maadili kama inavyosisitizwa katika imani za dini mbalimbali. Hii ni pamoja na suala zima la kutafuta elimu na maarifa ikiwemo kujifunza kuhusu dhana ya urasimishaji biashara. Hii ilitoa msukumo wa kuwa na ushirikiano pia na wasanii maarufu nchini akiwemo Bw. Emmanuel Mgaya – Masanja Mkandamizaji na mwimbaji wa nyimbo za Injili, Bi. Christina Shusho ili kuleta hamasa na kutoa elimu ya urasimishaji biashara kwa umma.

Aidha, Taasisi imeendelea kujiimarisha kwa kujitangaza kupitia majukwaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya maadhimisho ya Siku Maalum ya Miliki Ubunifu (IP Day), kushiriki katika maonesho na kufanya uhamasishaji kwa njia ya ukaguzi elimishi kwa wafanyabiashara, semina na mafunzo kwa makundi mbalimbali kama vile wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, wajasiriamali na wanafunzi wa vyuo na shule za sekondari nchini. Mbali na mafanikio yaliyoanishwa, wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wizara ya BRELA walipata fursa ya kushiriki mafunzo yaliyotolewa na Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute). Wakala kwa kutambua nafasi na dhima ya vyombo vya habari katika kuchochea maendeleo ya shughuli za urasimishaji biashara, ilitoa mafunzo kwa waandishi wa habari wa magazeti, runinga, redio na mitandao ya jamii.

Kwa ujumla, Toleo hili limeainisha masuala muhimu yaliyotekelezwa na BRELA ambayo ni chachu katika kuongeza uelewa na ari kwa msomaji kutaka kufahamu zaidi juu huduma za Taasisi hii. Hivyo nipende kukutakia usomaji mwema na kukaribisha maoni yako ili kutuwezesha kuboresha Jarida hili. Karibu sana.

**BODI YA UHARIRI**
**Andrew Mkapa** - Mwenyekiti
**Theresa Chilambo** - Katibu

**WAJUMBE**
Meinrad Rweyemamu
Tawi Kilumile
Abdul-rahman Twaha Songoro
Neema Kitala
Yusuph Nakapala
Tulizo Mpina
Stanslaus Kigosi

# BRELA YATOA GAWIO KWA SERIKALI KWA TAASISI ZA UMMA

Na Mwandishi Wetu







Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan amepokea gawio la zaidi ya Sh bilioni 18.9 kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ikiwa ni utekelezaji wa utoaji gawio kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370. Hafla ya kukabidhi gawio hilo la Sh18,973,853,514/27 imefanyika Juni 11, 2024 na kuhudhuriwa na Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Waziri kwa BRELA, Dkt Fred Msemwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw Godfrey Nyaisa.

# BRELA YASAINI MAKUBALIANO NA TAASISI NNE ZA SERIKALI

*Na Theresa Chirambo*



***PICHA:*** *Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (wapili kushoto), akiangalia bidhaa zinazotengenezwa na wabunifu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Miliki Ubunifu, Dar es Salaam).*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) wamesaini makubaliano na taasisi nne za Serikali wakikubalina kushirikiana ili kuleta ufanisi chanya hapa nchini.

Taasisi ambazo zimesaini makubaliano na Brela jijini Dar es salaam leo Mei 9, 2024 wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Miliki Duniani ni Chuo Kikuu Mzumbe, Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA).

Katika maadhimisho hayo, ambayo yamefanyika hapa nchini, Duniani kote ikiwa imefanyika Aprili 26, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sana na Michezo, Hamisi Mwinjuma akimwakilisha Waziri wa Viwanda na Biashara Ashatu Kijazi, amewataka BRELA na COSOTA kutoa elimu zaidi hususani kwa wabunifu ili wanafuike na kazi zao.

"Niwaelekeze BRELA na COSOTA wakae kwa pamoja waangalie namna ya kutoa wabunifu wakiwemo wasanii wachanga ili kutoa fursa ya kunufaika na kazi zao kutokana na elimu watakayokuwa nayo kuhusu Miliki Bunifu", amesema.

Aidha ameongeza kuwa BRELA wanatakiwa kuhakikisha wanajielekeza kuifanyia Miliki Bunifu inatambulika na wabunifu waweze kukopesheka tofauti na hivyo inaweza kutafsirika kama porojo.

Pia ameipongeza Taasisi ya



***PICHA:** Mstari wa mbele waliokaa kutoka kushoto ni: Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya BRELA Prof. Neema Mori, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Hamis Mwinjuma (katikati) Afisa Mtendaji Mkuu wa COSOTA Bi. Doreen Sinare na Mwenyekiti wa Bodi ya COSOTA Bw. Victor Michael Tesha na (Waliosimama kutoka Kushoto) ni: Mtendaji Mkuu wa TPHPA Profesa Joseph Ndunguru, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe Prof. William Mwegoha, Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Prof. William Pallangyo na mwakilishi wa Ruge Mutahagwa Foundation*

Ruge Mutahaba kuja na wazo la kupeleka elimu ya Miliki Bunifu kwa wasanii wadogo ambapo pindi watakapoelimima wataweza kuweka ulinzi kwenye kazi zao.

“Katika siku hii ya leo ni vema kupitia majadiliano yenu mnapata majibu ya changamoto zilizoko na kuziwasilisha wizarani kwa ajiliya kufanyiwa kazi ili tutakapokutana tena mwakani tuwe na jambo lingine la kufanya na si kurejea haya,” amesema.

Pia amebainisha kuwa Wizara inaendelea kufanya Mchakato wa kukamiisha sera ili kutoa mchango mkubwa katika sekta Bunifu.

Pia Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Godfrey Nyaisa, amesema kuwa elimu kuhusu Miliki Bunifu bado iko chini nchini hivyo wanaendelea kuelimu ili kufanikisha lengo husika.

Ameongeza kuwa katika kuhakikisha wanafikia malengo wamekuwa na utaratibu wa kutoa ufadhili kwa wafanyakazi wao kuendeleza na masomo ya katika kozi ya Miliki Bunifu ndani na nje ya nchi.

Katika shughuli hiyo, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Nyaisa na Naibu Waziri, Mwinjuma walikabidhi mfano wa hundi kwa wanufaika wanne wa masomo ya Miliki Bunifu ya sh. Milioni 16.5 Kwa kila moja.

# BRELA WATAKIWA KUFUNGUA MLANGO WA KUELIMISHA UMMA

*Na Christina Njovu*



Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania Dkt. Sheikh Abubakar Zubeir bin Ali Mbwana ameitaka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kutoa elimu kwa watu waielewe na kufaidika na huduma inazozitoa.

Sheikh Zubeir alitoa rai hiyo Aprili 3, 2024 katika hafla ya Iftar iliyoandaliwa na BRELA kwa wadau wake iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali na kufanyika Jijini Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo, Mufti alisema kwa kuwa wapo watu waliofungua kampuni bila kufahamu namna ya kusimamia, BRELA haina budi kuendelea kufungua milango ili watu wengi waifahamu taasisi yenyewe pamoja na shughuli inazoofanya ili kuwasaidia kufanya biashara kwa mujibu wa sheria.

"Taasisi itoe elimu kuhusu masuala ya BRELA kwa kuwa wapo watu wengi wanaoitaja Wakala, lakini hawajui inafanya nini. Kwa msingi huo, hivyo ni muhimu kuwaelimisha ili wafahamu huduma zinazotolewa, jinsi ya kuzipata na umuhimu wake," anasema Sheikh Zubeir.

Akieleza umuhimu wa elimu Sheikh Zubeir anafafanua mtu anaweza kuharibikiwa na mambo mengi asipokuwa na elimu huku akitanabaisha kuwa, ujinga ni aibu na hakuna anayeukubali na kuuridhia.

Katika hatua nyingine, Sheikh Zubeir anampongeza Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa kwa kuandaa Iftar kwa mara ya kwanza na kushukuru kwa kumwalika pamoja na wadau wengine kuwa watu wa kwanza kushiriki katika tukio hilo. Amewahimiza kuifanya kazi hiyo kuwa endelevu.

"Awali nilimuuliza Bw. Nyaisa hii ni Iftar ya ngapi kufanyika hapa. Akanieleza kuwa hii ni mara ya kwanza kufanyika kwa tukio kama hili. Nampogeza sana kwa kuandaa na ni imani yangu kwamba, mtaendelea kufanya vizuri zaidi," anasema Sheikh Zubeir.

Akimkaribisha Mufti katika hafla hiyo, Bw. Nyaisa alimshukuru Mufti na Sheikh Mkuu kwa kukubali kushiriki katika hafla ya Iftar ya kwanza kwa BRELA na kuahidi kuboresha zaidi sambamba na kuwakumbuka watu wenye uhitaji.

BRELA iliandaa Iftar hiyo kwa mara ya kwanza ili kuendelea kuwa karibu na wadau ambapo Mhe. Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Dkt. Sheikh Abubakar Zubeir bin Ali Mbwana alikuwa mgeni rasmi wa hafla hiyo.

Pamoja na hafla hiyo BRELA inatarajia kurudisha kwa jamii

# TANZANIA YASAINI MKATABA WA KIMATAIFA WA WIPO

*Na Mwandishi Wetu, Uswisi*



Tanzania imeungana na nchi wanachama wa Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO) kupitisha na kusaini Mkataba wa kihistoria wa kimataifa kuhusu Miliki Ubunifu, Rasilimali za Kijenetiki na Maarifa ya Jadi.

Mkataba huo unalenga kulinda haki za wenyeji asilia na jamii za kijadi katika kuhakikisha matumizi ya rasilimali za kijenetiki na maarifa ya jadi katika tafiti na vumbuzi yanaleta faida kwa jamii hizo.

Mkataba huo wa kihistoria na wa aina yake umejadiliwa kwa takribani miaka 25 na nchi wanachama wa WIPO kabla ya kupitishwa rasmi Mei 24, 2024 katika Mkutano wa Kidiplomasia uliofanyika katika Makao Makuu ya Shirika hilo Jijini Geneva, Uswisi.

Akiwa jijini Geneva, Uswisi, Balozi na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa (UN) na Mashirika ya Kimataifa, Mheshimiwa Dkt. Abdallah S. Possi aliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo wa Kidiplomasia uliopitisha Mkataba huo na kusaini Mkataba kwa upande wa Tanzania.

Walioshuhudia hafla ya utiaji saini mkataba huo ni Afisa Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa, Msajili wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea kutoka Wizara ya Kilimo, Bw. Twalib Njohole, Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu kutoka BRELA, Bi. Loy Mhando na Afisa Mambo ya Nje kutoka Ubalozi wa Tanzania Geneva, Bi. Zulekha Fundi.

Baada ya Mkataba huu kuridhiwa na nchi, BRELA na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) watakuwa na jukumu la kuhakikisha waombaji wa ulinzi wa vumbuzi kupitia Sheria za Hataza wanafichua taarifa za mahali zilipopatikana rasilimali za kijenetiki na maarifa ya jadi yaliyotumika katika tafiti na vumbuzi husika.

Jukumu lingine lilikuwa kufuatilia matumizi ya rasilimali hizo zinazopatikana hapa nchi ambazo watafiti na wavumbuzi kutoka nchi nyingine wanazitumia katika tafiti na vumbuzi zao ili kuhakikisha wamiliki wa rasilimali hizo hapa nchini wanapata faida zitakazotokana na matumizi ya rasilimali hizo.

Mkataba huu ulianza kutumika rasmi siku 30 baada ya nchi 15 kuwasilisha nyaraka za uridhiwaji wa Mkataba huo katika Ofisi za WIPO.

# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA KIDIPLOMASIA WA UKAMILISHWAJI SHERIA YA KIMATAIFA YA MILIKI UBUNIFU KATIKA RASILIMALI ZA KIJENETIKI

*Na Christina Njovu*




***PICHA:** Mhe Dkt Abdallah S. Possi, Balozi na Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Kimataifa (wa kwanza kushoto), Bw Godfrey Nyaisa Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA (katikati) na Bi Loy Mhando (wa kwanza kulia) wakifuatilia mkutano wa kidiplomasia wa ukamilishwaji sheria ya kimataifa ya miliki ubunifu katika Rasilimali za Kijenetiki*

Tanzania yashiriki mkutano wa kidiplomasia wa ukamilishwaji wa sheria ya kimataifa ya Miliki Ubunifu katika Rasilimali za Kijenetiki na Maarifa ya Jadi yanayohusiana na Rasilimali za Kijenetiki unaofanyika katika Ofisi za Makao Makuu ya Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO) kuanzia tarehe 13 Mei, 2024 hadi 24 Mei, 2024 jijini Geneva, Uswisi

Sheria hiyo ya Kimataifa inalenga kuhakikisha mfumo wa ulinzi wa Miliki Ubunifu unatambua matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki na Maarifa ya Jadi ili kuwanufaisha wamiliki wa rasilimali hizo

Ujumbe kutoka Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Balozi na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Kimataifa Dkt Abdallah Possi akiambatana na Afisa Mtendaji Mkuu kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa, Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA), Msajili wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea Wizara ya Kilimo Bw. Twalib Njohole, na Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu kutoka BRELA Bi. Loy Mhando

# KATIBU MKUU: WAFANYABIASHARA RASIMISHENI BIASHARA MFAIDIKE

*Na Christina Njovu, Morogoro*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah amewataka wafanyabiashara nchini kurasimisha biashara zao ili kuleta maendeleo, kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa. Hayo yamesemwa Juni 18,2024 katika mafunzo ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa waandishi wa habari yaliyofanyika Morogoro. Alisema biashara zikirasimishwa zitasaidia kukuza maendeleo nchini.




*PICHA: Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah akifungua mafunzo ya siku nne ya BRELA kwa waandishi wa habari wanaoripoti Mkoa wa Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalifanyika mjini Morogoro*

Alisema katika kutafsiri kwa vitendo dhamira, mweleko na Dira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na kama Wizara, walikaa na kuona kuna tatizo moja la habari kutokufika kwa usahihi na habari sahihi kuchelewa ufika kwa wakati sahihi, hivyo kupitia BRELA wameandaa semina maalum kwa waandishi wa habari.

Aidha, alisema lengo la kutoa mafunzo hayo kwa waandishi wa habari ni kuwafahamisha shughuli za msingi zinazofanywa na BRELA, sera za biashara zilizopo nchini na namna ya kurasimisha biashara kutoka kutokuwa rasmi.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo na kuwafahamisha majukumu yanayofanywa ndani ya Taasisi zao na yaliyofanywa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika falsafa nzima ya kuwekwa mazingira wezeshi na rahisi ya ufanyaji wa biashara nchini.

Aliongeza kuwa, katika mafunzo hayo washiriki watapata fursa ya kuchambua sheria sita zinazosimamiwa na BRELA ikiwemo miliki ubunifu, usajili wa biashara, urasimishaji wa biashara.

"Imani yetu kwamba mafunzo haya yatawanufaisha waandishi na kutoa elimu kubwa kwa wabunifu jamii na nchi




*PICHA : Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akizungumza wakati wa mafunzo ya BRELA kwa Waandishi wa Habari wanaoripoti Mkoa wa Dar es Salaam, yaliyofanyika mjini Morogoro*

kwa ujumla juu ya urasimishaji, ufanyaji biashara na uwekaji wa mazingira wezeshi unaofanywa katika biashara na uwekezaji ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," anasema.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa anasema wataendelea kufanya kazi kwa karibu na waandishi wa habari kuhakikisha umma unapata taarifa sahihi kutoka kwa Wakala hii.

Alisema mafunzo hayo ni moja ya utekelezaji wa maazimio yao ya kuhakikisha wanatoa elimu kwa umma kuhusu utendaji kazi wao na kuhimiza umma kurasimisha biashara zao.

Aidha, Nyaisa amesisitiza kuwa mafunzo hayo yatakuwa endelevu kwa waandishi wote nchi nzima kuhakikisha wanapata uelewa kuhusu Taassi hii na pia, kuhakikisha waandishi wanapata taarifa sahihi kutoka kwenye chanzo husika.

"Mafunzo haya yatakuwa endelevu na tutawafikia waandishi nchi nzima kwani matarajio yetu ni kuwa na mabalozi wazuri watakaoweza kuandika makala na taarifa sahihi ili kumwezesha mwananchi kuhamasika kurasimisha biashara yake na pia, tutaandaa tuzo kwa ajili ya waandishi watakaokuwa wamefanya vizuri katika uandishi wa habari zinazohusu shughuli za uchumi na biashara hususan zinazofanywa na BRELA," alisema Nyaisa.

# BRELA KUWAJENGEA UWEZO WAANDISHI WA HABARI

*Na Sheila Mfunami, Morogoro*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah amewashauri waandishi wa habari za biashara na uchumi kuendelea kuwafikishia wananchi taarifa sahihi zinazohusu Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Akifungua mafunzo ya siku nne yaliyoandaliwa na BRELA kwa waandishi wa habari na kufanyika Morogoro Juni 18, 2024 anasema BRELA imeandaa mafunzo maalumu kwa waandishi wa habari za biashara wa vyombo mbalimbali vya habari kutoka mkoani Dar es Salaam ili kuwajengea uwezo utakaowezesha kuandika kwa weledi habari za serikali hususani zinazohusu biashara.

Anasema wameanza na waandishi hao wa habari za biashara kutoka Dar es Salaam hasa wanaondika habari za BRELA, lakini mikakati uliopo ni kuwezesha mafunzo hayo kutolewa kwa waandishi wa mikoa yote ili kuhakikisha wanaendelea kuwajengea uwezo wadau muhimu wakiwemo waandishi wa habari wenzao.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa anasema Taasisi imeandaa mafunzo hayo ikiwa ni moja ya utekelezaji wa malengo ya Serikali ya kuhakikisha inatoa habari na elimu kwa umma na wadau mbalimbali nchini.

"Tumeshuhudia baadhi ya habari ambazo zinaripotiwa lakini zina makosa mengi. Namna ya kupunguza makosa hayo ya kiuandishi kwa habari za kibiashara ni kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wanahabari ili kuyaondoa," anasema.

Anasema kupitia wakurugenzi wa Wakala, watatoa elimu ya kutosha katika mafunzo hayo, hivyo waandishi wa habari wasisite kuuliza kujifunza na kupata uelewa zaidi.

Kwa mujibu wa Nyaisa, Mpango Mkakati wa BRELA ni kuwa na kanzidata ya waandishi wa habari wanaoandika habari za Wakala katika mukhtadha wa urasimishaji biashara ili kusaidia kuwa na habari sahihi na kwamba, mafunzo hayo yataendelea kutolewa sambamba na kuwaita katika matukio yanayohusiana na BRELA.

Anasema kuanzia sasa BRELA itaanza kutoa Tuzo Maalumu kwa waandishi wa habari za biashara watakaokuwa wakiandika makala zenye matokeo chanya kwa jamii sanjari na makala zitakazokuwa zimejitosheleza.

# BRELA YATOA ELIMU MAONESHO YA MIAKA 60 YA MUUNGANO




*Na Mwandishi Wetu*

*PICHA : Afisa Usajili wa Wakala wa Usajili wa Kampuni na Leseni (BRELA), Ruth Mbaga (kushoto) akitoa elimu kwa mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, Abibu Jitwe (kulia), alipofika kupata elimu katika banda la taasisi hiyo kwenye Maonesho ya Muungano jijini Dar es Salaam*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umeendelea kutoa elimu kwa wananchi mbalimbali waliotembelea Maonesho ya Miaka Sitini ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika Maonesho hayo, Afisa Usajili wa BRELA, Ruth Mmbaga anasema yanatoa fursa kwa wananchi kupata elimu juu ya kazi wanazofanya sambamba na kupata huduma za papo kwa hapo zikiwemo za usajili wa kampuni na majina ya biashara zao.

BRELA imekuwa na uhusiano mzuri na Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara Zanzibar, (BPRA) katika nyanja mbalimbali ikiwemo usajili wa Alama za Biashara na Huduma, Hataza na katika Leseni za viwanda na biashara kwa biashara zenye sura ya kitaifa na kimataifa.

Maonesho hayo ya wiki moja yalifunguliwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla mnamo Aprili 19, 2024 na kufungwa Aprili 25, 2024.






# BRELA YAPATA TUZO TAASISI BORA KIDIGITALI

*Na Lugano Mwakyombe*

WAKALA wa usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imepata tuzo katika kipengele cha taasisi bora ya Serikali kidigitali ikiwa ni kutambua mchango bora katika mageuzi ya kidigitali nchini Tanzania.

Tuzo hizo zimeandaliwa chini ya programu iitwayo Ufunguo Innovation inayosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo (UNDP) kwa kushirikiana na kampuni ya Serengeti Bytes na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) yenye lengo la kutambua michango mbalimbali inayotolewa na Taasisi za Umma na Sekta Binafsi nchini katika utoaji wa huduma kwa jamii.

Aidha, tuzo za kidigitali kwa mwaka 2023 zilienda sambamba na maadhimisho ya miaka 10 ya wiki ya ubunifu ikiangazia mafanikio na changamoto katika ubunifu wa kidigitali.




***PICHA:*** *Afisa Habari Mkuu wa BRELA, Bi. Christina Njovu akipokea tuzo kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu, Bw Godfrey Nyaisa kutoka kwa Naibu Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, Mhe. Balozi Mehdi Hussain baada ya kuitambulisha BRELA kuwa Taasisi Bora ya Serikali Kidigiti.*

# BRELA YAWASHIKA MKONO WATOTO WENYE UHITAJI - CHAKUWAMA

*Na Sheila Mfunami*




Katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetembelea Kituo cha Kulelea Watoto Wenye Uhitaji cha CHAKUWAMA kilichopo Sinza Dar es Salaam kuwafariji na kuwapa msaada wa vitu mbalimbali.

Akikabidhi msaada huo kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Mei Mosi, 2024, Afisa Habari Mkuu wa BRELA, Bi. Christina Njovu alisema taasisi hiyo imetoa msaada huo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya kurudisha kwa jamii. Alisema Wakala imekuwa ikitekeleza sera hiyo mara kwa mara katika taasisi na shughuli mbalimbali. Baadhi ya vifaa vilivyokabidhiwa katika kituo hicho ni pamoja na vyakula kama unga, sukari, vifaa vya usafi na vifaa mbalimbali vya shule.

Katika tukio hilo, Mkuu wa Kituo cha CHAKUWAMA, Bw. Hassan Hamis anaishukuru BRELA kwa kufika kituoni hapo kuwatembelea sambamba na kutoa msaada aliosema umewapa faraja kubwa.

Hivi karibuni kituo hicho kilikumbwa na janga la moto kwa kuunguliwa bweni la kulala watoto.Kwa mujibu wa Hamis, kituo hicho kina watoto 72 wa jinsi zote wenye umri kuanzia chini ya mwaka mmoja hadi miaka 19.

Anasema watoto wengi kituoni hapo wanasoma katika shule za msingi na sekondari na kwamba, changamoto zilizopo ni nyingi, hivyo msaada huo kutoka BRELA utapunguza ukali wa baadhi changamoto zinazowakabili.

Akielezea historia ya kituo hicho, Hamis anasema kilianza mwaka 1998 kikiwa na watoto watano chini ya mwanzilishi wake, Bi. Saida Hassan.

Anasema wakati huo kituo kilikuwa kikitumia nyumba ya kupanga iliyokuwa Mikocheni, Dar es Salaam. Kituo kimesajiliwa na kinafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Watoto na Makundi Maalum. Mkuu wa kituo huyo anafafanua kuwa, kituo chake kina watoto aliowatenga katika makundi sita wakiwemo yatima waliopoteza wazazi wote wawili na watoto waliopoteza mzazi mmoja.

Aidha, wapo watoto waliotolewa katika mazingira hatarishi na wale waliofanyiwa ukatili na waliookolewa kutoka katika biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu pamoja na watoto wenye ulemavu.

Hamis anaongeza kuwa, kati ya watoto 72, watoto 60 wanaosoma katika ngazi tofauti kuanzia chekechea, msingi na sekondari katika shule za serikali na shule binafsi, vyuo vya ufundi stadi vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na vyuovikuu na vya kati.

Amedokeza kuwa, miongoni mwa changamoto zinazowakabili ni pamoja na kuwapo watoto 12 ambao wamesimamishwa masomo kutokana na kuathirika kiakili kulikotokana na ukatili waliofanyiwa na wengine kupata magonjwa. Watoto hao wanaendelea kupata matibabu.

Mbali ya kutembelea kituo cha watoto wahitaji, BRELA ilishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani iliyobeba kaulimbiu: 'Nyongeza ya Mishahara ni Msingi wa Mafao Bora na Kinga Dhidi ya Hali Ngumu ya Maisha.'

# TUMIENI MAONESHO HAYA KUPUNGUZA CHANGAMOTO

*Na Sheila Mfunami, Tanga*

Wafanyabiashara nchini wametakiwa kutumia fursa ya maonesho ya biashara na utalii kupunguza kero mbalimbali zinazojitokeza zikiwemo urasimishaji wa biashara pamoja na uhuishaji wa taarifa za kampuni.

Afisa Sheria wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Lupakisyo Mwambinga amesema hayo wakati akihudumia wateja waliojitokeza kwenye banda la BRELA katika Uwanja wa Usagala uliopo mkoani Tanga wakati wa Maonesho ya 11 ya Biashara na Utalii Mwaka 2024.

“Maonesho haya ni muhimu, ukizingatia kwamba hivi sasa masuala ya uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji likiwemo suala la usajili wa majina ya biashara na kampuni, usajili wa alama za biashara na huduma pamoja utoaji wa leseni za biashara na viwanda yanafanyika kwa njia ya mtandao kupitia mifumo ya kielektroniki au mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), hivyo ni vyema wadau wakajitokeza kwa wingi kupata huduma za BRELA,” anasema Mwambinga.

Katika mazungumzo hayo Mei 30, 2024, anasema maonesho ni chachu kwa wafanyabiashara ambao hawajasajili biashara zao na kuhuisha taarifa za kampuni zao. BRELA inawawezesha kutoa usaidizi wa karibu kwa wanaofanya mabadiliko mbalimbali ya usajili




*Afisa Sheria wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Lupakisyo Mwambiga wakati akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kwenye maonyesho ya 11 ya Biashara na Utalii yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule ya Sekondari Usagara Jijini Tanga.*

Aidha,alitumia nafasi hiyo kuwakaribisha wadau kufika katika banda la BRELA ili kupata huduma za papo kwa papo.

Anaongeza kuwa, ushiriki wa BRELA katika maonesho hayo kwa wafanyabiashara ni nyenzo ya kupunguza kero na changamoto mbalimbali zinatokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha wa mifumo ya usajili.

Maonesho ya 11 ya Biashara na Utalii (Tanga Trade Fair -2024) yameandaliwa na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga.

# BRELA YAITA WAFANYABIASHARA KUJISAJILI, KUCHANGAMKIA FURSA

*Na Sheila Mfunami, Tanga*



***PICHA:** Afisa Sheria wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Lupakisyo Mwambinga akizungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya 11 ya Biashara na Utalii yaliyofanyika katika Uwanja wa Shule ya Sekondari Usagara jijini Tanga*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umewataka wafanyabiashara kuchangamkia fursa kwa kujisajili ili wawe na sifa za kushiriki na kuomba zabuni zinazotangazwa na taasisi mbalimbali za serikali na idara zake.

Afisa Sheria wa BRELA, Bw. Lupakisyo Mwambinga anabainisha hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya 11 ya Biashara na Utalii yaliyofanyika katika Uwanja wa Shule ya Sekondari Usagara iliyopo Tanga.

Kwa mujibu wa Mwambinga, ameeleza kuwa endapo hujasajiliwa hataweza kuomba zabuni zinazotangazwa na taasisi mbalimbali za serikali na idara zake hivyo, ni vema wafanyabiashara na wajasiriamali kuona umuhimu wa kurasimisha biashara zao kwa kusajiliwa na BRELA na kupata leseni inayostahili ili wachangamkie fursa za kibiashara.

"Wengi wanachanganya leseni kati ya daraja A na B ambazo zinatolewa na Halmashauri. Kuna Leseni za biashara zenye sura ya kitaifa na kimataifa ambazo ni za Kundi A zinazotolewa na BRELA hivyo unatakiwa kupata leseni ya biashara kutoka BRELA" amesema

Ameongeza kwa kuwahimiza wafanyabiashara waje kupata elimu hii kwa kueleza biashara wanazofanya ili waelimishwe na kushauriwa leseni wanazopaswa kuomba kutoka BRELA.

Ameendelea kusema kwa wafanyabiashara wenye viwanda vidogo, BRELA inatoa leseni za viwanda na watu wengi hawana ufahamu kuwa unapoanzisha kiwanda lazima uwe na leseni kutoka BRELA

Amehitimisha kwa kuwaalika wafanyabiashara wenye changamoto kutembelea banda lao ili waone na kujua mahitaji na mambo wanayopaswa kufanya ili kupata leseni.



# BRELA KUENDELEA KUIMARISHA UHUSIANO NA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM ( UDSM )

*Na Lugano Mwakyombe*

Wakala wa usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetoa pongezi kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuadhimisha wiki ya Utafiti na Ubunifu ambayo iliambatana na Maonesho ya Tafiti na Bunifu mbalimbali zinazofanywa na wadau kutoka katika chuo hicho.

Akizungumza katika hafla ya kuhitimisha Maadhimisho hayo tarehe 07 Juni, 2024 katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bi Loy Mhando ambaye ni Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu amesema, BRELA itaendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutokana na mchango wake mkubwa wa kuendeleza Bunifu na Tafiti mbalimbali zinazofanywa na wahadhiri na wanafunzi chuoni hapo.

Katika Maadhimisho hayo yaliyohudhuriwa na viongozi, wadau wa maendeleo, wawakilishi kutoka taasisi za Umma na binafsi, wahadhiri, watumishi na wanafunzi wa kada Mbalimbali wa chuo hicho wameelezwa namna wanavyoweza kutumia bunifu zao kutatua changamoto katika jamii, vile vile kujikwamua kiuchumi na kutengeneza fursa za ajira kwa wengine.

Washiriki wamepata fursa ya Kukumbushwa kuwa nyenzo za Miliki Ubunifu ni mali kama mali nyingine na inapolindwa inakuwa na thamani inayoweza kuleta faida nyingi kwa wabunifu na Taifa kwa ujumla. Bi. Mhando ametoa rai kwa Chuo na wabunifu kuhakikisha wanalinda kazi zao kwa kupitia BRELA ili waweze kunufaika na kazi zao pamoja na kuepuka hasara ya bunifu zao kuhujumiwa na watu wengine.

Aidha, ameeleza kuwa, katika eneo la kukuza na kuhamasisha ubunifu nchini, BRELA inatekeleza jukumu muhimu kati ya majukumu yake ambalo ni ulinzi wa bunifu na kurasimisha biashara nchini kwa kusajili Kampuni, Majina ya Biashara na kutoa Leseni za Biashara, kwa kutambua hilo, BRELA imesaini hati ya makubaliano ushirikiano MoU) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kama sehemu ya ushirikiano huo, BRELA imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa Shahada ya Umahiri ya Miliki Ubunifu (Master of Intellectual Property - MIP) ambao idadi yao ni 14 mpaka toka kuanzishwa kwakwe mwaka 2020.

Katika tukio hilo muhimu la Maadhimisho ya Wiki ya Utafiti na Ubunifu, BRELA imetoa ufadhili wa Tuzo moja wapo kati ya Tuzo zilizotolewa ambayo ni katika kipengele cha ‘Mradi bora wa Ubunifu kutoka shahada ya kwanza.

# BRELA YAELEZA SIRI YA MAFANIKIO HUDUMA RAFIKI BILA TAHARUKI

*Na Mwandishi Wetu, Morogoro*



*PICHA: Waandishi wa habari wa Mkoa wa Dar es Salaam waliohudhuria mafunzo yaliyoandaliwa na BRELA wakimsikiliza Mkurugenzi wa Leseni, Bw. Andrew Mkapa (hayupo pichani) akiwasilisha mada yake Juni 18, 2024 katika Hotel ya Morena mjini Morogoro.*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeeleza siri ya mafanikio kufanya kazi zake bila kusabababisha usumbufu au taharuki kwa jamii kuwa ni pamoja na kutoa huduma zake kwa mtazamo wa kirafiki.

Akizungumza Juni 18, 2024 wakati akitoa mada kuhusu utoaji wa leseni za biashara kundi A kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Dar es Salaam waliohudhuria mafunzo ya siku tano mjini Morogoro, Mkurugenzi wa Leseni BRELA, Bw. Andrew Mkapa ameeleza namna Taasisi inavyotoa huduma kwa mtazamo wa kirafiki zaidi na kwamba, hiyo ndio maana halisi ya kuwa Wakala kwa niaba ya Serikali.

Katika ufafanuzi wake, Bw. Mkapa anasema: "Kuna swali limeulizwa hapa kwa nini hatuna kishindo na nini siri ya mafanikio yetu? BRELA tunatoa leseni za biashara ambazo ni za kundi A zenye sura ya kitaifa na kimataifa, hivyo hatuna ofisi katika ngazi ya chini kabisa, lakini tunakwenda kutoa elimu kwa wananchi."

Anaongeza kuwa, wanapokwenda mikoani hushirikiana na maofisa biashara wanaohusika kutoa leseni na kuwapa elimu.

Anasema siri kubwa ya mafanikio ya BRELA ni kubadilika kimtazamo kwa sababu nia kubwa ya Serikali ilikuwa kubadilisha taasisi hizi kuwa Wakala.

"Serikali ilitoa jukumu la kusimamia kwa niaba yake na lengo la kutoa nafasi kwa Wakala ilikuwa ni kupunguza urasimu. Hii imesaidia katika kutoa huduma zetu," Kwa mujibu wa Mkapa, mafanikio ya Taasisi na kutoa huduma kirafiki yametokana na kubadilika kwa fikra kulikoifanya Wakala kufanya kazi zake kiweledi zaidi.Kuhusu utoaji wa leseni za biashara kundi A, Bw. Mkapa anasema awali leseni hizo zilikuwa zikitolewa moja kwa moja na Wizara ya Viwanda na Biashara lakini, jukumu hilo lilihamishiwa BRELA.

Anasema zipo aina mbili za leseni zinazotolewa na BRELA ikiwemo leseni ya biashara kundi A ambayo imekaa katika sura ya kitaifa na kimataifa na leseni za viwanda.

Mkurugenzi huyo wa Leseni anasema tangu mwaka 2018/2019 huduma za BRELA zinatolewa kupitia mtandao, hivyo mtu anaweza kuomba leseni ya biashara bila kulazimika kwenda ofisini.

Anasisitiza akisema wakati jukumu la kutoa leseni kundi A zinahahamishwa kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, kulikuwa na mfumo uliobakia kidogo wa kukamilisha kwa ajili ya mfumo wa kutoa leseni za biashara kwa njia ya mtandao.





“Mfumo ulianza kutengenezwa wizarani na ulikuwa umefika hatua za mwishoni lakini na BRELA ilianza kutengeneza mfumo wake kwa ajili ya kutoa huduma ilizokuwa nazo,” anasema.

Anaongeza: “Hivyo, BRELA ilikuwa na mfumo na ndio maana mfumo wa wizarani unatumika katika leseni za biashara za kundi A na zinapatikana katika mfumo wa Tanzania National Bussiness Portal (TNBP) kupitia www.bussiness.go.tz...”

Mkapa anawadokeza washiriki wa mafunzo hayo kuwa, huo ni mfumo mpana zaidi ulitengenezwa si tu kwa ajili ya kutoa leseni za kundi A, bali pia kutoa taarifa nyingine muhimu. Mfumo wa BRELA ulikuwepo unaunganishwa kupitia kiunganishi (link) ambayo ukibonyeza inakupeleka katika mfumo ulioanzia wizarani.

# WANACHUO DARTU WASHAURIWA KUFUATA SHERIA USAJILI BIASHARA

*Na Gerald Nyang’ali*






Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (DarTu) wameshauriwa kufuata sheria za usajili wa majina ya biashara, kampuni na huduma nyingine za kibiashara zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ili kuondoa usumbufu wanapoanzisha biashara baada ya kuhitimu masomo chuoni hapo.

Wito huo umetolewa Juni 21, 2024 katika mafunzo maalumu kuhusu umuhimu wa urasimishaji biashara na ulindaji wa bunifu mbalimbali yaliyotolewa na BRELA. Katika mafunzo hayo, Kaimu Mkuu Sehemu ya Hataza kutoka BRELA, Bi. Neema Kitala.

Anawashauri wanafunzi hao kupata taarifa sahihi za huduma za BRELA kupitia mitandao inayotumiwa na taasisi kufikisha taarifa kwa umma ili kuondokana na dhana kuwa taratibu za usajili zina mlolongo mrefu

"Kwa sasa ninyi ni wanafunzi, wengine mkitoka hapa mnaweza kuanzisha biashara na utakapokuwa mfanyabiashara hakikisha unazingatia taratibu za urasimishaji biashara unayofanya kwa njia ya mtandao," anasema.



Awali, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (DarTu), Profesa Burton Mwamila aliipongeza BRELA kwa kutoa elimu kwa kundi muhimu ambalo ni wanafunzi wa vyuo vikuu nchini kuhusu umuhimu wa urasimishaji wa biashara. Profesa Mwamila anaahidi kuendelea kutoa ushirikiano zaidi hasa katika nyanja ya ullindaji wa bunifu na vumbuzi za vijana. "Ni muhimu wanafunzi wakafahamu sheria na taratibu za usajili pamoja na uanzishaji wa biashara ili kuondoa changamoto zinazojitokeza pindi wanapoanzisha biashara au kampuni zao," anasema. Anaongeza: "Tumeanzisha programu ya kuwasaidia wanafunzi kuchunguza matatizo kwenye jamii na kuyatengenezea mawazo ya biashara yatakayoshindanishwa ili kuboreshwa katika mpango biashara kutokana na tatizo halisi la jamii…."

Anabainisha kuwa, washindi watakaopatikana kutokana na ushindani wa mawazo bunifu hayo watawekwa kwenye kituo atamizi chuoni hapo na kutapata ushauri wa namna ya kuendeleza biashara zao ikiwa ni pamoja na kupewa elimu mbalimbali namna ya kushughulikia biashara.

Mafunzo hayo yamehudhuriwa na wanafunzi wapatao 500 wa vitivo mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam.

# MATUNDA YA MIAKA 60 YA MUUNGANO FAIDA NNE SHERIA KUKUTANISHWA, MAFANIKIO LUKUKI MILIKI UBUNIFU

*Na Christina Njovu*



Nchi hizo huru, ziliungana Aprili 26,1964 ndipo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akawa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Sheikh Abeid Aman Karume, akawa Makamu wa Rais.

Akizungumzia miaka 60 ya Muungano, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa anasema kuundwa kwa sheria hiyo kumewezesha pande mbili za Muungano kufanya kazi pamoja na sasa inasimamiwa na kutekelezwa kwa pamoja baina ya BRELA na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar.

Anasema uanzishwaji wa sheria hiyo ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda, awali ulilenga kusimamia viwanda vya upande wa Tanzania Bara pekee, lakini mwaka 1982, ilifanywa kuwa ya Muungano baada ya kufanywa marekebisho katika Katiba na kuongezwa Leseni za Viwanda na Takwimu kwenye orodha ya mambo ya Muungano.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu huyo wa BRELA, marekebisho ya sheria hiyo yameleta mafanikio manne makubwa

katika miaka sitini ya muungano kwa kufanikisha utekelezaji wa usajili na utoaji wa leseni za viwanda nchini.

Mafanikio hayo ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda imeendelea kufanyiwa marekebisho kwa kuifanya ya kisasa zaidi inayozingatia na kuendana na hali halisi ya ufanyaji biashara ya sasa.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, alieleza kuwa mabadiliko yaliyotokea ni pamoja na kuhamisha idhini ya utoaji wa leseni za viwanda kutoka kwa Bodi ya Leseni za Viwanda kwenda kwa Msajili wa Viwanda, kufuta Kamati za Ushauri za Mikoa na jukumu lake la kushauri kuhusu viwanda kuhamishiwa kwa Bodi ya Leseni za Viwanda.

Nyaisa anasema lingine ni kuongezwa kwa kifungu kinachoeleza kuhusu uteuzi, idadi na taratibu za uendeshaji wa Bodi ya Leseni za Viwanda na kuboresha maana ya maneno mbalimbali yanayotumika kwenye Sheria hiyo kama vile maana ya Kiwanda.

"…Kujengwa kwa mfumo wa pamoja wa kielektroniki utakaotumika kutolea Leseni za Viwanda na Vyeti vya Usajili kwa pande zote mbili za Muungano ili kusaidia utekelezaji wa Sheria hiyo na kurahisisha upatikanaji wa takwimu za viwanda za nchi nzima ni sehemu ya mabadiliko hayo," anasema.

Nyaisa anafafanua; "Mabadiliko mengine ni kufanyika kwa vikao vya pamoja vya ushirikiano baina ya pande mbili za



Muungano vilivyojadili masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa Sheria hii hasa mfumo ya kielektroniki vilivyotoa ufumbuzi wa pamoja wa changamoto nyingi kwa manufaa ya pande zote mbili za Muungano."

Kwa mujibu wa BRELA, kufanyika marekebisho ya jedwali la ada kwa kubadilisha malipo ya ada za leseni na usajili wa viwanda kutoka katika Dola za Marekani na kuwa katika Shilingi za Tanzania, hivyo kupanua wigo wa urasimishaji wa viwanda, hasa viwanda vidogo.

Wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari, wakifuatilia mkutano ulioandaliwa na BRELA kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wakala hiyo.

Katika umri huo wa miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, BRELA kwa kushirikiana na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) zimekuwa na mafanikio makubwa katika eneo la Miliki Ubunifu.

Kupitia BRELA na BPRA zinazosimamia Miliki Ubunifu Tanzania Bara na Zanzibar, mafanikio lukuki yamepatikana yakigawanyika katika ngazi tatu yaani kitaifa, kikanda na kimataifa ndani ya miaka 60 ya Muungano.

**Mafanikio Kitaifa**

Kwa mujibu wa BRELA, ushirikiano mzuri na wa karibu katika ubadilishanaji wa taarifa, kushirikishana ujuzi na uzoefu baina yake na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) umeziwezesha taasisi hizo kupiga hatua kubwa katika utendaji kazi wake, lengo likiwa kutoa huduma haraka, kwa ubora, weledi na ufanisi.

Aidha, ushirikiano huo umezifanya BRELA na BPRA kuwa na mifumo inayofanana katika uchakataji na ushughulikiaji wa maombi ya Alama za Biashara na Huduma pamoja na Hataza.

BRELA ilieleza kuwa mifumo hiyo ya kielektroniki inajulikana kama, Mfumo wa Usajili kwa

Njia ya Mtandao (Online Registration System - ORS) pamoja na mfumo wa kuchakata na kuhifadhi maombi ya Miliki Ubunifu (Intellectual Property Automated System (IPAS).

Mafanikio Kikanda BRELA inadokeza kuwa, mwaka 1976 Tanzania ilijiunga na Shirika la Miliki Ubunifu la Kanda ya Afrika (African Regional Intellectual Property Organization-ARIPO). Kupitia ARIPO, taifa limesaini na kuridhia Itifaki katika Usimamizi wa Maeneo Mahsusi ya Miliki Ubunifu.

Itifaki zilizoridhiwa na manufaa yaliyopatikana ni pamoja na Tanzania kusaini na kuridhia Itifaki ya Harare ya Ulinzi wa Hataza na Maumbo Bunifu (Harare Protocol on Protection of Patents and Designs) mwaka 1982. Hatua hiyo iliwezesha wabunifu kulinda bunifu zao ikiwa ni Hataza na Maumbo Ubunifu hivyo kuongeza wigo wa ulinzi wa bunifu husika.

Aidha, Tanzania ilisaini Itifaki ya Banjul ya Ulinzi wa Alama Mwaka 1993, (Banjul Protocol on the Protection of Marks 1993) inayotoa fursa kwa Wabunifu wa Alama (nembo) kusajili na kupata ulinzi wa Alama za Biashara na Huduma kwa kupitia ARIPO, hivyo kuongeza wigo wa ulinzi kwa wabunifu husika.Mwaka 2015 Tanzania pia ilisaini Itifaki ya Arusha ya Ulinzi wa Mbegu Mpya za Mimea. Itifaki hiyo inatoa fursa kuongeza wigo wa ulinzi kwa wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Vilevile, mwaka 2021 Tanzania ilisaini Itifaki ya Kampala ya Usajili wa Hiyari wa Hakimiliki na Hakishiriki inayotoa fursa kuongeza wigo wa ulinzi wa wabunifu wa kazi za sanaa na uandishi.

Kama hiyo haitoshi, mwaka 2023 Tanzania ilisaini Itifaki ya Ulinzi wa Haki za Miliki Ubunifu chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (Protocol on Protection of Intellectual Property Rights under the African Continental Free Trade Area - AfCFTA).Kwa kuwa mwanachama wa Shirika hili, Tanzania imenufaika katika mambo mbalimbali ikiwamo kujengewa uwezo na kuongeza ujuzi na utaalam katika eneo la Miliki Ubunifu na kujifunza kutoka nchi nyingine wanachama.

Aidha, kutoa elimu kwa kuanzisha Shahada ya Umahiri katika Miliki Ubunifu inayotolewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Kimataifa**

Mwaka 1983, Tanzania ilijiunga na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (World Intellectual Property Organization – WIPO). Kupitia Mkataba wa Stockholm, uanachama wa Tanzania WIPO, umeliwezesha taifa kujiunga na mikataba inayohusiana na usimamizi na uratibu wa masuala mbalimbali yanayohusu Miliki Ubunifu.

Mikataba iliyojiunga nayo ni pamoja na ule wa Paris wa Ulinzi wa Mali Ubunifu (Paris Convention for Protection of Industrial Property of 1883), Mkataba wa Berne wa ulinzi wa Kazi za Uandishi na Sanaa (The Berne Convention for the Protection of Literary and Artistic Works of 1886), Mkataba wa Nice wa Madaraja ya Alama za Biashara na Huduma (Nice Agreement concerning the International Classification of Goods and Services of 1957) na Mkataba wa Ushirikiano wa Hataza (The Patents Cooperation



Treaty - PCT of 1970).

Tanzania imejiunga pia na Mkataba wa Masuala ya Ulinzi wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea unaojulikana kwa jina la Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (International Convention for the Protection of New Varieties of Plants chini ya International Union for the Protection of New Varieties of Plants).

Mbali na mikataba hiyo, Tanzania pia ni mwanachama wa Shirika la Biashara Dunia (WTO). Kupitia uanachama huo, inatakiwa kutekeleza Mkataba wa Masuala ya Miliki Ubunifu yanayohusiana na Biashara wa mwaka 1994 (Trade-Related Aspects of Intellectual Property Agreement -TRIPS of 1994 of the World Trade Organization).

Kwa mujibu wa BRELA, mkataba huo unatoa nafuu na fursa katika eneo la Miliki Ubunifu.

Fursa hizo ni pamoja na uwezekano wa kutumia teknolojia za dawa na vifaa tiba zinazopatikana katika Hataza (Patent) unaowezesha pia upatikanaji rahisi wa dawa na vifaa tiba kwa bei nafuu au kutumia teknolojia hizo pasipo kupata matatizo ya kisheria kutoka kwa wamiliki wa teknolojia husika.

Kwa mujibu wa BRELA kupitia mikataba hiyo ya kikanda na kimataifa ya uratibu na usimamizi wa Miliki Ubunifu, Tanzania imenufaika kwa kuongeza ujuzi kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu, uhawilishaji wa teknolojia, kubadilishana ujuzi katika masuala ya Miliki Ubunifu na kuwezesha kuongeza wataalamu wa Miliki Ubunifu.

Aidha, imenufaika kwa kukuza uelewa wa matumizi ya Miliki Ubunifu kwa maendeleo endelevu na kuboresha mifumo ya usimamizi na uratibu wa Miliki Ubunifu kwa pande zote mbili za Muungano.

# MILIKI UBUNIFU NA UKUZAJI WA BIASHARA KIKANDA NA KIMATAIFA

*Na Mwandishi wetu*

Katika makala zilizotangulia tuliangalia dhana ya Miliki Ubunifu na umuhimu wake katika biashara, uchumi na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Tuliona ni kwa namna gani Miliki Ubunifu ni mojawapo ya nyenzo muhimu katika maendeleo ya binadamu.

Umuhimu kwa mtu mmoja na Taifa kwa ujumla.
Uwepo wa sheria na sera madhubuti zinazoweza kusimamia ulinzi na uvunaji wa rasilimali hii adhimu ijulikanayo kama Miliki Ubunifu.
Kama ilivyoeleza awali, Miliki Ubunifu ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya binadamu na katika kudhibiti ushindani wa kibiashara katika mawanda ya kikanda na kimataifa. Mfano mzuri ni kama wa matumizi ya alama za biashara na huduma namna zinavyoweza kutumika kujijenga kibiashara na kujenga himaya imara katika biashara.

Aidha, matumizi ya alama za biashara na huduma yanaweza kutumika na washindani wako kibiashara kama silaha ya kubomoa na kuharibu biashara yako kwenye soko kama utakuwa hujachukua hatua muhimu za kuzilinda alama zako za biashara au huduma.

Ili mtu aweze kujijenga kibiashara na kujenga himaya yake katika biashara jambo la kwanza analopaswa kufanya ni kuhakikisha alama yake ya biashara inatambulika na kuaminika sokoni. Hii huambatana na kupeleka bidhaa au huduma bora kwa walaji.

Mfanyabiashara akifanikiwa katika hili, walaji wa bidhaa na huduma zake huanza



kutumia bidhaa au huduma kutokana na uaminifu uliojengeka katika alama ya bidhaa au huduma zinazotolewa na mfanyabiashara husika.

Washindani wa kibiashara wakiona kwamba kuna alama inayofanya vizuri sana sokoni, jambo la kwanza hufanya uchunguzi kujua kama alama husika ya biashara au hudumaimesajiliwa na kupata ulinzi wa kisheria.
Ikitokea wakagundua kwamba mmiliki wa alama husika ya biashara au huduma hajaipatia ulinzi wa kisheria kwa kuisajili, basi jambo la kwanza wanalofanya ni wao kukimbilia kuisajili.

Wakifanikiwa kufanya usajili huo, wanakuwa na mambo mawili wanayoweza kufanya. Jambo la kwanza ni kumzuia mmiliki halisi wa alama hiyo ya biashara au huduma kuitumia kwa kuwa wao wanakuwa ndio wamiliki halali kisheria wa alama hiyo maana wamefanikiwa kuisajili na kupata umiliki halali wa kisheria.

Jambo la pili washindani hao wa kibiashara wanaloweza kufanya ni kuanza kuzalisha bidhaa na huduma zisizo na ubora kama zile bidhaa halisi za mmiliki wa alama ya biashara au huduma ambaye hakuweza kusajili alama yake ya biashara.

Inapotokea likafanyika jambo la pili, basi ule uaminifu ambao walaji wa bidhaa au huduma zilizokuwa zinatolewa chini ya alama ambayo haikuwa imepata ulinzi wa kisheria, wateja wataacha kutumia bidhaa au huduma zile maana zitakuwa ni shida sana kutofautisha bidhaa halisi na zinazozalishwa na watu ambao si wazalishaji au waanzilishi asilia wa bidhaa na huduma husika.

Matokeo yake, yule mmiliki wa alama ya biashara na huduma ambayo haikuwa imepata ulinzi atalazimika kuondoka sokoni kwa kukosa walaji wa bidhaa na huduma zake.

Hili linapotokea, si tu kwamba mmiliki wa biashara anakuwa amepata hasara, bali serikali pia itakuwa imepoteza mojawapo ya vyanzo vyake vya mapato.

Hata zile ajira zilizokuwa zimezalishwa katika biashara hiyo zitakuwa zimepotea.

Mnyororo wa hasara za kutosajili alama ya biashara au huduma ni mkubwa kwa maana unavuruga kabisa ikolojia ya biashara na ushindani wa biashara.

Sasa turudi kwenye mada ya makala hii kwa nini Miliki Ubunifu ni muhimu kwenye maendeleo ya biashara kimataifa? Tanzania imeridhia mikataba mbali ya kikanda na kimataifa kuhusu biashara.

Mikataba hii inaposainiwa huwa inafungua milango kwa wafanyabiashara wa mataifa mengine kuja kufanya biashara hapa nchini. Aidha, mikataba hiyo huwa inafungua milango kwa wafanyabiashara wa Tanzania kwenda kuwekeza na kufanya biashara katika mataifa ambayo tumeingia

nayo mikataba hiyo.

Umoja wa Afrika (AU) kupitia mkataba wake wa the African Continental Free Trade Area (AfCFTA) wa mwaka 2018 umeanzisha Eneo Huru la Biashara Afrika ili kuunganisha nchi wanachama wa AU kuweza kufanya biashara ndani ya Bara la Afrika bila vikwazo.

Tanzania ikiwa mwanachama wa AU, imesaini mkataba huu, hivyo Tanzania ambayo ni mojawapo ya nchi zilizosaini mkataba huu imefungua milango yake kuruhusu wafanyabiasha wengine kutoka katika nchi wanachama wa AU kufanya biashara ndani ya Tanzania bila vikwazo.

Halikadhalika, wafanyabiashara wa Tanzania wapo huru kwenda kufanya biashara na uwekezaji kwenye nchi nyingine zilizosaini mkataba huu.

Mojawapo ya maeneo muhimu ambayo yamewekewa msisitizo katika ufanyaji biashara katika Eneo Huru la Biashara Afrika ni masuala yote yanahusu Miliki Ubunifu.

Kama ilivyoelezwa katika aya zilizotangulia, Miliki Ubunifu inaweza kutumika kama kizuizi cha kumfanya mshindani wa kibiashara asiingie kwenye soko ambalo mwingine yupo.

Ikumbukwe kuwa, mojawapo ya kanuni muhimu za ulinzi wa kazi za Miliki Ubunifu huishia kwenye mipaka ya nchi husika (territorial protection).

Usipolinda kwa kusajili kazi yako ya Miliki Ubunifu ndani ya nchi fulani, maana yake ni kwamba huo ubunifu wako unauacha huru kwa mtu mwingine ndani ya nchi hiyo kuweza kuutumia atakavyo ikiwa ni pamoja na kuhujumu biashara yako ili usifanikiwe kupeleka ushindani katika soko husika.

Hivyo, ni muhimu kwa sasa nchi inapozidi kufungua milango ya kuruhusu wawekezaji kuja kuwekeza na kufanya biashara Tanzania, wafanyabiashara wa




Tanzania wanaotaka kwenda kufanya uwekezaji kwenye mataifa mengine kuona ulazima wa kwenda kulinda kazi zao ambazo zinaangukia kwenye Miliki Ubunifu kuhakikisha zinalindwa katika zile nchi wanazotamani kwenda kuwekeza na kufanya biashara.

Bila kufanya hivyo, washindani wao kwenye soko watakwenda kulinda ubunifu katika maeneo hayo hivyo kujikuta wafanyabiashara wa Tanzania wanashindwa kuyafikia masoko ya nje ya Tanzania. Kwa wale ambao watakuwa wanapata changamoto namna ya kuingia na kufanya usajili wa kazi zao za Miliki Ubunifu nje ya Tanzania, ni vema wakafanya mawasiliano na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ambao ndio Ofisi ya Taifa ya Miliki Ubunifu kupata ushauri na mwongozo wa namna bora ya kulinda ubunifu wao nje ya Tanzania.

# HABARI NA MATUKIO KATIKA PICHA




**Rais Samia apokea gawio la Bil 18.9/- kutoka BRELA**

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan (katikati) Juni 11, 2024, alipokea gawio la kiasi cha TZS. Bilioni Kumi na Nane Mia Tisa Sabini na Tatu, Millioni Mia Nane Hamsini na Tatu Elfu, Mia Tano Kumi na Nne na Senti Ishirini na Saba tu (18,973,853,514.27) kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ikiwa ni utekelezaji wa utoaji gawio kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370. Hafla hiyo ilihudhuriwa na Dkt. Fred Msemwa (kushoto) Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wizari kwa BRELA na Bw Godfrey Nyaisa Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA (kulia).*





*Afisa Mtendaji mkuu wa BRELA wakibadilishana hati za makubaliano na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe Prof. William Mwegoha baada ya kutia saini wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Miliki Ubunifu yaliyofanyika tarehe 9 Mei, 2024 jijini Dar es Salaam*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa wakiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) Prof. Joseph Ndunguru, baada ya kusaini hati ya makubaliano ya ushirikiano baina ya taasisi hizo mbili Mei 9, 2024 jijini Dar es Salaam*




***PICHA :*** *Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Hamis Mwinjuma (aliyekaa katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa BRELA Prof. Neema Mori (wa pili kushoto), Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa (wa tatu kushoto). Kulia kwa mgeni rasmi ni Afisa Mtendaji wa Ofisi ya Haki Miliki Tanzania (COSOTA), Bi. Doreen Sinare, Mwenyekiti wa Bodi ya COSOTA Bw. Victor Michael Tesha na baadhi ya watumishi wa BRELA (waliosimama) baada ya kufungua rasmi Maadhimisho ya Siku ya Miliki Ubunifu Duniani yaliyofanyika katika Hoteli ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam).*



***PICHA :*** *Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Hamis Mwinjuma akikabidhi hundi ya mfano kwa Bw Calvin Rwambogo mnufaika wa ufadhili wa shahada ya Uzamili wa Miliki Bunifu inayotolewa katika Chuo kikuu cha Dar es SalaaM*



***PICHA :*** *Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akipokelewa na wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa BRELA pamoja na Menejimenti ili kushiriki kikao cha upokeaji wa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa BRELA Kikao kazi kilifanyika Mei 15, 2024 katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*



***PICHA :*** *Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akisaini kitabu cha wageni alipotembelea ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam tarehe 15, Mei 2024 Mei 15, 2024.*







***PICHA :*** *Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akipokea taarifa ya utekelezaji wa Wakala kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa BRELA, Profesa Neema Mori na Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Bw. Andrew Mkapa. Kikao kazi kilifanyika Mei 15, 2024 katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*



***PICHA :*** *Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akiwa katika picha ya pamoja na Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa BRELA pamoja na Menejimenti.*



*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akiwa amekutana na wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa BRELA pamoja na Menejimenti wakati akipokea taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa BRELA katika kikao kazi kilichofanyika Mei 15, 2024 katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*




















*Wamiliki wa Wake Up Women Investment wakipokea cheti cha usajili (Partnership) baada kukamilisha taratibu zote za usajili BRELA Aprili 25, 2024 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam wakati wa Maonesho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar*




*Mtaalamu wa TEHAMA wa BRELA, Bw. Fadhil Mlosa akitoa huduma za usaidizi kwa wamiliki wa Wake Up Women Investment walipofika kufanya usajili wa jina la biashara katika Viwanja vya Mnazi mmoja jijini Dar es Salaam wakati wa Maonesho ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar*








BRELA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
Huduma zifuatazo zinapatikana BRELA:-
1 Usajili wa Kampuni
Usajili wa Majina ya Biashara
Usajili wa Alama za Biashara na Huduma



# COSOTA, BRELA WAINOA TASUBA

*Na Sheila Mfunami, Bagamoyo*

Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) wametoa mafunzo katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) iliyopo Bagamoyo mkoani Pwani kuhusu Miliki Ubunifu.

Mafunzo hayo yaliyotolewa TaSUBa kama sehemu ya maandalizi ya kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Miliki Ubunifu Duniani.Katika mafunzo hayo wanafunzi wameelezwa huduma mbalimbali zinazotolewa na BRELA sambamba na masuala muhimu kama Alama za Biashara na Huduma, Hataza pamoja na elimu ya Hakimiliki.

Akizungumzia huduma zinazotolewa na BRELA katika mafunzo hayo, Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Hataza, Bi. Neema Kitala amewataka wanafunzi hao wasisite kurasimisha biashara zao ili kuongeza wigo wa kutambulika na mamlaka mbalimbali na hata kuwawezesha kukopesheka katika taasisi za fedha.
Meneja Idara ya Kumbukumbu na Usajili wa COSOTA, Bw. Philemon Kilaka amewasisitiza wanafunzi wa TaSUBa kusajili kazi zao za ubunifu katika Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ili wanufaike na kazi zao.

“Urasimishaji una faida nyingi ikiwemo usimamizi wa kazi zenu kwa ufanisi, kulindwa na sheria ya Hakimiliki na kupata fursa za biashara zaidi kwa kuwa mtakuwa mnatambulika. Vilevile, mtaweza kuongeza kipato binafsi na cha Taifa kwa ujumla, pamoja na kupanua soko la kazi zenu”, anasisitiza Kilaka.

Katika mafunzo hayo ya siku moja mjini hapa, Afisa Sheria wa BRELA, Bw Calvin Rwambogo amewahimiza wanafunzi hao kuchukua hatua kwa kuanza mchakato wa kusajili bunifu zao BRELA kabla ya kupeleka katika jamii ili kuepuka kuibiwa bunifu husika.

Mbali na TaSUBa, BRELA imefikisha elimu ya Miliki Ubunifu katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Innovation Hub ya Taasisi ya Afya ya Ifakara na Kiatamizi (Incubator) cha Ubunifu kijulikanacho kama TAOTIC. BRELA inaendelea kutoa elimu hii katika vyuo mbalimbali nchini.





***PICHA :*** *Wanafunzi wa Taasisi ya Sanaa na Ubunifu (TaSUBa) waki-wasikiliza wataalamu wa Miliki Ubunifu na Hakimiliki kutoka BRELA na COSOTA (hawapo pichani) Mei 2, 2024 mjini Bagamoyo*



Afisa kutoka BRELA Bw. Calvin Rwambogo (kushoto) na Bw. Benedickson (kulia) wakitoa ufafanuzi kwa wanafunzi wa TaSUBa wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya miliki ubunifu

# WANANCHI: HUDUMA ZA MTANDAONI BRELA ZIMEPUNGUZA VISHOKA

*Na Gloria Mbilimonywa*

Uboreshaji na utoaji wa huduma za Wakala wa Usajili wa Kampuni na Leseni (BRELA) umesaidia na kumewawezesha wananchi wengi kuzifikia na kuzipata hali iliyoondoa kwa kiasi kikubwa changamoto za 'vishoka'.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika jijini Dar es Salaam, wananchi mbalimbali waliofika katika Banda la BRELA kupata huduma zinazotolewa na taasisi hiyo wamesema matumizi ya mfumo wa kimtandao wa BRELA yamewandolea kwa kiasi kikubwa adha ya kukumbana na vishoka.

"Kwa kweli huduma za BRELA za mwaka 2012 na sasa ziko tofauti sana, kwani sasa wameboresha huduma zao kupitia mfumo wa mtandao unaomsaidia mwananchi kufanya usajili mwenyewe na hivyo, kumaliza malalamiko ya wananchi hususani kuhusu suala vishoka waliokuwa wakiwatapeli pesa zao," anasema Mwenyekiti Mstaafu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Jacob Mwakasoye.

Naye mwanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), Emmanuel Mishapiti anaonesha kuridhishwa kwake na huduma zitolewa na BRELA akisema taasisi hiyo, imemwezesha kusajili jina la biashara katika sekta ya utalii ambayo ni fani anayosomea.

"Tumefanikiwa kusajili jina la biashara ya fani tunayosomea ya utalii na baadae tutasajili kampuni itakayotuwezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi zaidi," anasema Mishapiti.

Afisa Leseni wa BRELA, Koyan Aboubakar anasema katika maonesho hayo zaidi ya wananchi 200 wamehudumiwa na kupewa vyeti vya usajili papo hapo.

Anatoa rai kwa wananchi kuacha kuwatumia watu kati maarufu, vishoka badala yake, watumie mfumo wa kimtandao kupata huduma za BRELA haraka na kwa uhakika zaidi.

Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka huu yamefikia yakiongozwa na kaulimbiu: 'Kuwekeza kwa Utumishi wa Umma wa Afrika Karne ya 21 iliyo jumuishi na inayostawi; ni safari ya mafunzo na mabadiliko ya kiteknolojia' yametamatishwa Juni 23, 2024 ambapo kitaifa yamefanyika jijini Dodoma.



# 'SAJILINI BIASHARA ZENU BRELA MFAIDIKE'

*Na Lugano Mwakyombe, DODOMA*




*PICHA: Kaimu Meneja Rasilimali na Utawala BRELA, Migisha Kahangwa akizungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kitaifa katika Viwanja vya Chinangali Park, Dodoma.*

Kaimu Meneja Rasilimali na Utawala wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Migisha Kahangwa amewahimiza wananchi kusajili biashara zao BRELA ili ziwe rasmi na kutambulika.

Kauli hiyo imetolewa wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali Park jijini
Aliendelea kusema kuwa kila mwananchi ana haki ya kutoa huduma kwa maana ya kufanya biashara ili kuwa na uhakika ni muhimu kujisajili.

Katika hatua nyingine, Kahangwa anabainisha kuwa, ili kukabiliana na changamoto hiyo BRELA wamekuwa wakitioa elimu kwa wananchi kutumia huduma za Taasisi hiyo, hivyo ni muhimu wachangamkie fursa ya elimu kupitia maonesho hayo ya Wiki ya Utumishi wa Umma kupata elimu kuhusu huduma wanazotoa.

Afisa Usajili wa BRELA, Gabriel Girangay anasema BRELA imekuwa ikitoa elimu kwa wanachi kuhusu huduma inazozitoa huku akiwashauri wananchi kujaza Fomu Namba 128 kwa ajili ya kutoa taarifa kuhusu usajili wao kama unafanya kazi au la.

Gilangay alifafanua kuwa, mtu asipojaza fomu hiyo wao (BRELA) hawawezi kujua kama biashara aliyoisajili inafanyika au la na hatimaye, wanaweza kuwafuta au kuwaondoa kwenye mfumo.

# HATUWEZI KUMLINDA ASIYESAJILI JINA LA BIASHARA - BRELA

*Na Christina Njovu na Sheila Mfunam*

Katika kuhakikisha wanaendelea kurahisisha utoaji huduma, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imesema kupitia mfumo wa kimtandao wa ORS unaoweza kupata huduma zao zikiwemo za kufanya usajili wa kibiashara kama leseni ya kiwanda au kusajili ukiwa mahali popote.
Mkurugenzi wa Leseni wa BRELA, Andrew Mkapa anasema hayo wakati akiwasilisha mada kuhusu Leseni za Viwanda pamoja na usajili.

Anasema kupitia mfumo wa mtandao, mtu anaweza kupata leseni au kusajili kiwanda akiwa mahali popote hata akiwa nyumbani.

"Kupitia mfumo wa kimtandao ambao BRELA tunao, tumerahisisha sana upatikanaji wa huduma zetu; hakuna haja ya kuja ofisini maana unaweza kupata usajili wa leseni ya biashara kundi A, kupata leseni ya kiwanda na kusajili kiwanda kidogo kwa kutumia mtandao tu," anasema.
Anafafanua: "Ukiwa na simu kubwa yenye uwezo, utaingia katika Mfumo wa BRELA na kufanya usajili. Kikubwa ni kuwa na viambatanisho muhimu vinavyohitahijika pamoja na aandiko linalohusu kiwanda husika."
Mkapa anasema viwanda vikubwa na vya kati hupewa leseni wakati viwanda vidogo husajiliwa.

Anasema viambatanisho ni utambulisho wa mmiliki anapotakiwa kuwa na nyaraka au hati mbalimbali zinazoelezea eneo ambalo kiwanda kitakuwepo, uwezo wake kimtaji kwa maana ya uwekezaji na hivyo vyote vitaonekana kupitia andiko na nyaraka nyingine zitakazokuwa zimetolewa na taasisi nyingine.

Kuhusu leseni ya viwanda, Mkapa anasema viwanda vimegawanyika katika makundi mawili kwa mujibu wa sheria. Kundi la kwanza, anasema ni viwanda vikubwa na vya kati ambavyo mtaji wake unaanzia Sh. milioni 100 na kundi la pili linahusisha viwanda vidogo ambavyo mtaji wake ni chini ya Sh. milioni tano.

Kwa mujibu wa Mkapa, ada ya usajili wa leseni ya kiwanda ni Sh. 800,000 na ada hiyo inalipwa mara moja tu kwa kipindi chote cha uhai wa kiwanda lakini kwa upande wa viwanda vidogo, ada ya usajili ni Sh 10,000 na hiyo ni kwa muda wote.

"Leseni ya viwanda vikubwa ni Shilingi 800,000.00, halafu kiwanda ambacho uwekezaji wake hauzidi Shilingi milioni, ni Shilingi za Tanzania 10,000.00. Uwekezaji unaozidi Shilingi milioni tano ada yake ni Shilingi 50,000 na uwekezaji unaozidi Shilingi milioni 10 ada yake ni Shilingi 100,000," anasema.

Anasema baada ya kiwanda kupewa leseni au kusajiliwa, kila mwaka wahusika wanapaswa kuwasilisha taarifa za maendeleo ya kiwanda na kwamba, ipo fomu maalumu ya kujaza inayouliza juu ya maendeleo ya kiwanda.

"Ripoti hii ya kiwanda inayotakiwa kuwasilishwa BRELA kila mwaka haina malipo katika kiwanda. Ni bure kama ukitoa taarifa ndani ya mwaka, lakini ukichelewa ndio kuna faini ndogo kama Shilingi 10,000," anasema.

Anaongeza: "Lakini tunaamanisha wenye viwanda ambao wamepata leseni kutoa taarifa zao kwani zinasaidia kutunza kumbukumbu zinazoweza kutumiwa na Serikali," anasema.

Mkapa anasisitiza umuhimu wa kufanya hivyo akisema ndio maana Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza taasisi za Serikali kusomana kimtandfao, badala kuingia katika mfumo wa kila mmoja.

"Hivyo na BRELA tumeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine, lakini mfumo huo una matoleo mengine kwa taasisi inayotaka kuingia katika mfumo wetu ili kurahisisha huduma.

Hata hivyo BRELA tumejipanga kuendelea kutoa huduma bora sambamba na kuendelea kurasimisha viwanda," anasema.

Anasema mkakati wa BRELA ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma wanayoifanya hauzidi siku tatu na kama ombi litakuwa limekamilika na hakuna maombi mengi kwa siku hiyo, hata saa moja au mbili zinatosha kukamilisha huduma.

# RC TANGA AIPONGEZA BRELA



Mkuu wa Mkoa wa Tanga Balozi. Dkt. Batilda Salha Burian, ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa kazi za uboreshaji miundombinu ya utumiaji wa mfumo wa Usajili kwa njia ya mtandao (ORS), ambao umewezesha kuwafikia wafanyabiashara wengi na kukuza uchumi wa nchi leo tarehe 03 Juni 2024 Jijini Tanga.

Mhe. Balozi Dkt.Burian ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la BRELA katika maonesho ya Biashara ya 11 ya Utalii-Tanga Trade Fair 2024 yanayofanyika katika viwanja vya shule ya Sekondari Usagala Jijini Tanga na kupata maelezo kuhusu majukumu na mchango wa Taasisi hiyo katika kuboresha mazingira ya biashara nchini.

“Naomba mzidi kuwa mabalozi wazuri na msisite kutoa elimu zaidi ya kuwaleta sehemu moja wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi, ili kuongeza kasi ya uwekezaji pamoja na kukuza pato la Taifa na kuinua uchumi wa nchini”, amesisitiza Mhe. Dkt.Batilda.

Akiwa katika banda la BRELA, Mkuu huyo wa Mkoa wa Tanga alipokelewa na kupewa maelezo mafupi na Afisa Usajili wa wakala hiyo Bi. Julieth Kiwelu ambapo alimueleza kuhusu huduma mbalimbali zitolewazo sambamba na jukumu la kusimamia sheria za Usajili wa Majina ya Biashara, Kampuni, Usajili wa Alama za Biashara na Huduma, Utoaji wa Hataza na kutoa Leseni za Biashara kundi A, kutoa Leseni za Viwanda na kusajili Viwanda vidogo kwaajili ya kusaidia jitihada za Serikali za kuboresha ukuaji wa Uchumi.

BRELA imekuwa miongoni mwa taasisi za Serikali zinazoshiriki maonesho ya 11 ya Biashara na Utalii Tanga Trade Fair -2024 yaliyoanza tarehe 28 Mei,2024 na yanatarajia kufungwa ramsi tarehe 6 Juni 2024 Jijini Tanga ambapo mamia ya wananchi wamekuwa wakihudhuria katika viwanja hivyo kwa ajili ya kupata elimu kuhusu huduma zitolewazo na BRELA.

Maonesho hayo ambayo yamendaliwa chini ya Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga na yamehusisha Taasisi mbalimbali za masuala ya Biashara ambapo yameongozwa na kauli mbiu, “Kuchochea Uwekezaji na Biashara kwa Uchumi Endelevu




*Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt Hashil Abdallah, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA na Wakurugenzi kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara na BRELA wakiwa katika picha ya pamoja na waandishi wa habari kutoka Dar es Salaam walioshiriki mafunzo ya BRELA mkoani Morogoro*

Na Christina Njovu na Sheila Mfunami, Morogoro

Katika kuhakikisha wanaendelea kurahisisha utoaji huduma, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imesema kupitia mfumo wa kimtandao wa ORS unaoweza kupata huduma zao zikiwemo za kufanya usajili wa kibiashara kama leseni ya kiwanda au kusajili ukiwa mahali popote.
Mkurugenzi wa Leseni wa BRELA, Andrew Mkapa anasema hayo wakati akiwasilisha mada kuhusu Leseni za Viwanda pamoja na usajili.

Anasema kupitia mfumo wa mtandao, mtu anaweza kupata leseni au kusajili kiwanda akiwa mahali popote hata akiwa nyumbani.

"Kupitia mfumo wa kimtandao ambao BRELA tunao, tumerahisisha sana upatikanaji wa huduma zetu; hakuna haja ya kuja ofisini maana unaweza kupata usajili wa leseni ya biashara kundi A, kupata leseni ya kiwanda na kusajili kiwanda kidogo kwa kutumia mtandao tu," anasema.
Anafafanua: "Ukiwa na simu kubwa yenye uwezo, utaingia katika Mfumo wa BRELA na kufanya usajili. Kikubwa ni kuwa na viambatanisho muhimu vinavyohitahijika pamoja na aandiko linalohusu kiwanda husika."
Mkapa anasema viwanda vikubwa na vya kati hupewa leseni wakati viwanda vidogo husajiliwa.

Anasema viambatanisho ni utambulisho wa mmiliki anapotakiwa kuwa na nyaraka au hati mbalimbali zinazoelezea eneo ambalo kiwanda kitakuwepo, uwezo wake kimtaji kwa maana ya uwekezaji na hivyo vyote vitaonekana kupitia andiko na nyaraka nyingine zitakazokuwa zimetolewa na taasisi nyingine.


Kuhusu leseni ya viwanda, Mkapa anasema viwanda vimegawanyika katika makundi mawili kwa mujibu wa sheria. Kundi la kwanza, anasema ni viwanda vikubwa na vya kati ambavyo mtaji wake unaanzia Sh. milioni 100 na kundi la pili linahusisha viwanda vidogo ambavyo mtaji wake ni chini ya Sh. milioni tano.

Kwa mujibu wa Mkapa, ada ya usajili wa leseni ya kiwanda ni Sh. 800,000 na ada hiyo inalipwa mara moja tu kwa kipindi chote cha uhai wa kiwanda lakini kwa upande wa viwanda vidogo, ada ya usajili ni Sh 10,000 na hiyo ni kwa muda wote.

"Leseni ya viwanda vikubwa ni Shilingi 800,000.00, halafu kiwanda ambacho uwekezaji wake hauzidi Shilingi milioni, ni Shilingi za Tanzania 10,000.00. Uwekezaji unaozidi Shilingi milioni tano ada yake ni Shilingi 50,000 na uwekezaji unaozidi Shilingi milioni 10 ada yake ni Shilingi 100,000," anasema.

Anasema baada ya kiwanda kupewa leseni au kusajiliwa, kila mwaka wahusika wanapaswa kuwasilisha taarifa za maendeleo ya kiwanda na kwamba, ipo fomu maalumu ya kujaza inayouliza juu ya maendeleo ya kiwanda.

"Ripoti hii ya kiwanda inayotakiwa kuwasilishwa BRELA kila mwaka haina malipo katika kiwanda. Ni bure kama ukitoa taarifa ndani ya



# UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA KAMPUNI BAADA YA USAJILI

Msajili wa Makampuni anapenda kuwataarifu Wamiliki, Wakurugenzi na Makatibu wa makampuni kwamba baadhi ya makampuni yamekuwa hayatekelezi wajibu wao wa kisheria wa kuwasilisha kwa Msajili wa Makampuni Taarifa za Mwaka na Mizania **(Annual Returns and Audited Accounts)** za Kampuni kama Sheria ilivyoelekeza.

Sheria pia, inayataka Makampuni ya Kigeni **(Foreign Companies)** kuwasilisha Mahesabu yake ya Mwaka kila mwisho wa mwaka **(Calendar Year)**.

Taarifa hizi zinatakiwa kuwasilishwa kwa Msajili wa Makampuni kila ifikapo tarehe na mwezi ambao kampuni ilisajiliwa (anniversary of incorporation) au tarehe nyingine yoyote ambayo Kampuni itakuwa imeichagua na kumtaarifu Msajili wa Makampuni nae akaridhia. Sharti hili ni kwa mujibu wa **Kifungu cha 128** cha Sheria ya Makampuni, **Sura 212**.

Msajili wa Makampuni anapenda kuwafahamisha na kuwakumbusha kwamba, kuanzia sasa, Taarifa za Mabadiliko yoyote yanayoletwa na kampuni hayatafanyiwa kazi mpaka Kampuni husika itakapokuwa imewasilisha Taarifa zake za Mwaka.

Taarifa za Mwaka na Mahesabu ya Mwaka kwa kampuni za kigeni **(Foreign Companies)** husaidia kutoa taswira halisi ya Kampuni, hivyo humuwezesha Msajili wa Makampuni kuwa na taarifa sahihi za Kampuni husika. Makampuni yanahimizwa kuwasilisha Taarifa za Mwaka ili kuepuka usumbufu unaoweza kutokea wakati kampuni inawasilisha taarifa za mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika kampuni.




Kitalu Na. 20,
Kiwanja Na. 23Sokoine
Drive / Mtaa wa Shaaban Robert
S.L.P 9393, 11101, Dar es Salaam,
simu: +255 22 2212800Barua
Pepe: ceo@brela.go.tz
usajili@brela.go.tz
Tovuti: www.brela.go.tz

**JENGO LA BRELA**

@brela_tanzania
@brela_tanzania
@brela_tanzania
www.brela.go.tz

eMrejesho
***150*00#**
CHAGUA 9, KISHA 2

Pakua eMrejesho kwenye
GET IT ON Google Play